

Ukweli Hauna Kutu

# Pambazuko

Toleo Namba 023

Jumatatu Disemba 19-24, 2022

AJALI YA PRECISION AIR

## Mawakili wa nje waja kusaidia manusura

- Nao wanataka  
kulipwa asilimia 33



**...Waguswa waanza kulipwa ml.11.7/-**

Uk. 12



## Hakuna kuonewa tena-Nape

Uk. 6

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye  
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

## **Dkt. Samia, Nape timizeni ahadi**

**S**IYO mara moja ama mbili, bali mara nyingi tu, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amekuwa akieleza nia ya serikali ya awamu ya sita - inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa na utayari wa wazi kufanya kazi na vyombo vya habari.

Amenukuriwa mara kadhaa akizungumza mbele ya umma wa Watanzania na dunia, kwamba Rais Dkt. Samia amekuwa akisisitiza kuwekwa mazingira yenye kuwapa fursa waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa uhuru bila kubughudhiwa na vyombo vya usalama ama taasisi za serikali anayoiongoza.

Wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani zilizofanyika Arusha - kwa upande wa Afrika, Dkt. Samia alisema kuwa serikali anayoongoza itahakikisha inaweka mazingira mazuri kwa waandishi wa habari kufanya kazi zao, huku akieleza kufuatwa kwa maadili ya tasnia hiyo kwa kuandika ukweli na kutoonea mtu.

Hata hivyo, pamoja na ahadi hizo nzuri, bado kuna ukakasi ambao unaweza kukwamisha nia - tunayoamini ni nzuri, ya Rais Dkt. Samia na serikali yake; kutokuwepo kwa sheria na sera zinazolinda hayo wanayotamani yawepo au kuonekana yapo kwenye tasnia ya habari.

Bila kuwemo kwenye sheria, sera, kanuni na miongozo mingine, upo uwezekano wa tasnia ya habari, hata kama inafanya kazi kwa weledi na kufuata sheria za

nchi, ikashindwa kutoa mchango wake mkubwa kwa nchi kwa kuogopa kutishwa, kufungiwa, kupelekwa mahakamani kwa sababu za hovyoyo na wakati mwingine waandishi kuangukia kwenye tishio la kunyang'anywa haki yao ya kuishi.

Ikumbukwe kuwa vyombo vya habari vya Tanzania vilipitia nyakati ngumu zaidi kupata kutokea kwenye historia ya nchi hii; kipindi cha utawala wa Rais John Magufuli ambaye aliamua kuwa mbabe kwa vyombo vya habari.


Pamoja na nia tunayoiona kuwa njema ya kuwapa haki waandishi wa habari, ni vyema serikali ikaharakisha mchakato wa kuwepo sera na sheria ambayo itabeba hayo anayoahidi Rais Dkt. Samia na msaidizi wake, Waziri Nape.

Ieleweke kuwa kuwepo kwa sera na sheria zisizokandamiza utendaji wa waandishi wa habari, ni dhahiri maendeleo ya Tanzania yataongeza kasi kwani mchango wa sekta ya habari ni mkubwa mno, hata kama haupigwiwi 'chapuo' na wanasiasa wengi.

Pambazuko linaamini kuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mpenda haki, hivyo anakwenda kusimamia jambo hili lifanyike mapema naye apate mwanya wa kutambua yanayoendelea nje ya wigo rasmi wa kupokea taarifa na habari za utendaji wa serikali na hata maeneo mengine.

Uhuru wa vyombo vya habari, ni maendeleo dhahiri ya Tanzania. Ukumbatiwe.

3



## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

**NUKUU**



*“Uhuru wa habari lazima ulindwe kwa sheria badala ya utashi wa viongozi ili kiongozi yeyote alazimishwe kufuata sheria hiyo.”*

*- Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:*

*Desemba 17, 2022, Dar es Salaam.*

---

## **Ugumu wa maisha unamgusa Samia?**

**Na Plato Hekimachius**

**H**AKUNA ubishi kwamba Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuwa sehemu ya serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi wa John Pombe Magufuli. Wakati huo Samia akiwa Makamu wa Rais wa Tanzania.

Wakati wa kampeni katika uchaguzi mkuu wa 2015 na uliofuata wa 2020, Samia alimnadi Magufuli naye alimnadi Samia. Walishinda uchaguzi.

Sasa Samia Suluhu Hassan ni rais wetu. Alichaguliwa Magufuli, lakini baadaye tukampata Samia. Siamini kama kuna aliyempigia Samia ili kumpata Magufuli.

Rais Samia aliingia madarakani nchi ikiwa imevimba na kuishiwa pumzi. Vichaka na fukwe zilinuka damu na mahabusu za magereza zilijaa wafungwa. Ilifika mahali kila ofisi ya mteule wa Magufuli ilitumika kama mahabusu. Uhuru ulipotea na furaha kutoweka.

Samia alikuwa sehemu ya urithi huo, lakini Watanzania ni wepesi wa kusamehe na kusahau. Kwake rais wetu wa sasa, Dkt. Samia - hili ni deni lisilolipika.

Kiuchumi, Magufuli aliwakamua wafanyabiashara kodi kubwa kwa nguvu. Akazitumia kodi hizo kufanya mambo mazuri na mabaya, lakini alijitahidi jambo moja muhimu ambalo ni deni kwa Samia.

Rais Magufuli alijionyesha kuwakingia kifua wananchi maskini wasiteswe na kodi na tozo. Hivi sasa wananchi wengi wanateseka kwa ugumu wa maisha. Kila kitu kimepanda bei kuanzia chakula, gharama kubwa za bidhaa hata zinazolalishwa nchini.

Pamoja na gharama za maisha kuwa kubwa, bado wananchi wanadai kuwepo kwa mdodoro wa huduma kutoka ofisi, taasisi na mashirika ya serikali.

Wananchi wanalia kuwepo kwa ukomavu wa rushwa karibu kila mahali. Kwamba 'wanalipishwa' rushwa kama kodi. Hofu ya rushwa imetoweka nchini



*Rais Samia Suluhu Hassan*

na ofisi za umma ni mashindano ya kudai na kupokea rushwa.

Tuhuma za rushwa ni kubwa mno, kwenye baadhi ya hospitali rushwa inaanzia getini, shuleni ni rushwa, ukifika Polisi ni kama kosa kutotoa rushwa, mahakamani nako - karibu sasa wanaweka bei ya kila huduma kwenye ubao!

Kibaya zaidi ni kuwa zile sauti za watetezi zilizokuwa zikisikika wakati wa Magufuli ni kama zinatoweka. Vyombo vya habari, wanaharakati, vyama vya upinzani, viongozi wa dini na haki za binadamu wako kimya.

Hiki kimya hakilingani na madai ya uhuru wakati wa Magufuli. Iteleweke kwamba amani wakati wa Rais Samia hailingani na mateso wakati Magufuli. Hili ni deni kubwa lisilolipika.

Hali halisi ya maisha kwa sasa imejaa ugumu unaoelezwa na kuonekana kwa wananchi wengi ambao wanateseka chini ya utawala mzuri.

Ni wakati muafaka sasa kwa Rais Dkt. Samia kuangalia namna nzuri ya kukomesha kila aina ya uonevu na rushwa, ili nchi isiendelee kuzongwa na vilio vya ugumu wa maisha. Anaweza.

## Mwigulu anatuonaje Watz?

**Na Bullet RUHINDA**

**K**UKUA au kutokua kwa deni la taifa limekuwa suala la mjadala mkubwa kati ya wananchi katika majukwaa mbalimbali – hasa katika mitandao ya kijamii na majukwaa mengine sogozi.

Inawezekana kukukua kwa deni hilo ni mtazamo ambao kila mmoja ana wake. Wananchi wanaambiwa deni limekua kubwa sana, huku watawala wanasema linahimilika. Hiyo tutaachie wenyewe kwanza, angalau kwa sasa.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba, ni daktari wa uchumi na mchumi daraja la kwanza kama anavyopenda kujinasibu kila anapozungumza na vyombo vya habari au kuwa kwenye kadamnasi na Watanzania hatuna wasiwasi na usomi wake, ila tunakuwa na wasiwasi na maneno yake pale anapotuelezea kuhusu deni la taifa - hasa uhusika wa kila Mtanzania katika ulipaji wake.

Kwa maoni yangu, Dkt. Mwigulu Nchemba anatumia usomi wake kutuona wananchi wote au wengi hatuna tunachokijua kuhusiana na uchumi, hususan deni la taifa.

Kwa nyakati tofauti, amesikika akisema kwamba hakuna Mtanzania atakayegongewa mlango kuombwa kulipia deni la taifa! Wengi tulishangazwa na kauli hiyo kutolewa na mtu mwenye dhamana kubwa katika nchi. Hivi anatuonaje Watanzania? Kwamba sisi ni mbumbumbu kiasi cha kutojua kwamba deni la taifa linalipwa vipi?

Daktari huyo wa uchumi anataka kutuaminisha kwamba deni hata likikua kiasi gani, basi halituhusu, lakini kesho atakuja kutuambia mishahara haipandi kwa sababu ya uchumi mdogo (mbaya), hakuna ajira kwa sababu serikali haina uwezo wa kulipia ajira mpya, je, hajui kwamba kila Mtanzania analipia deni kwa kukosa dawa na matibabu kati hospitali zetu?

Je, hajui kwamba kila mzazi ambaye mwanee amekosa mkopo wa elimu ya juu amelipia deni? Anaposema hakuna



*Dkt. Mwigulu Nchemba*

atakayegongewa mlango ana maana gani?

Je, anaposema deni linalipwa na serikali na siyo wananchi maana yake nini? Serikali ni ya nani kama siyo sisi wananchi wenyewe? Je, kauli hizo za waziri zinalenga nini? Kutufurahisha na kutupaka mafuta kwa mgongo wa chupa kwamba deni halituhusu?

Tunapenda kumshauri Dkt. Nchemba kwamba anapotoa kauli zinazouhusu uchumi wetu, atambue kuwepo kwa maumivu tunayoyapata kutokana na deni la taifa na asijaribu kupima kiwango cha uelewa wa Watanzania.

Siyo kweli kwamba Watanzania hatuna uelewa wa mambo yanayojili katika uchumi. Tunaelewa na tunasikitishwa na hali hiyo, hivyo tusiongezewe uchungu mwingine kwa kauli nyepesi za kutusahaulisha ukweli wa jambo lenyewe kwamba kila Mtanzania anahusika kulipia deni la taifa, akiwama yeye – hata kama anapata fursa nyingine ambazo wengine hawapati kwa nafasi yake.

Dkt. Nchemba asitumie vyeti vyake kutuaminisha kwamba ni yeye tu mwenye uelewa mpana wa uchumi, hivyo ana haki ya kuendelea kutuhadaa.

---

## Hakuna kufinywafinywa tena - Nape

Na Asha MABRUKI

**S**ERIKALI imewahakikishia waandishi wa habari nchini Tanzania usalama, maslahi na uhuru wa kufanya kazi zao bila “kufinywafinywa.”

Mbali na kutoa ahadi hiyo, ambayo wengi wanaamini itasimamiwa vyema zaidi, endapo kutakuwepo na sheria, serikali imehimiza waandishi wa habari kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa weledi, kufuata sheria na kulinda maadili ya Mtanzania.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ametoa ahadi hiyo – kwa mara nyingine, huku akiwahakikishia waandishi, wamiliki wa vyombo vya habari na wadau wa sekta ya habari kuwa marekebishi ya sheria ya huduma za habari yatafanyika mwaka kesho - Januari 2023.

Nape ameyasema juzi – Jumamosi Desema 17, 2022 jijini Dar es Salaam wakati akifungua kongamano la kwanza la maendeleo ya sekta ya habari lililoandaliwa na wizara hiyo na kuwakutanisha wadau zaidi ya 1000 wa sekta hiyo.

Waziri huyo ambaye aliwahi kuhudumu kwenye nafasi hiyo wakati sekta ya vyombo vya habari ikikumbwa na madhila kadhaa ya kuonewa, kutishwa, kupelekwa mahakamani kwa kesi za kubumba na kufungiwa vyombo vya habari – miaka sita iliyopita, amesema ili taifa liwe na maendeleo, furaha na amani ni lazima kuwepo kwa uhuru wa habari.

“Hakuna furaha, amani na maendeleo kama uhuru wa habari katika jamii hiyo haupo hivyo ni muhimu kulinda uhuru wa habari ili vitu hivi viwepo kwenye jamii. Hilo linawezekana na huo ndio msingi wa kongamano hili ambalo linalenga kuleta maendeleo, furaha na msingi wa taifa letu.

Waziri Nape alisema sheria na kanuni kadhaa zinaendelea kufanyiwa mabadiliko kwa mujibu wa sheria na kwamba uhuru



**Waziri Nape Nnauye**

wa habari lazima ulindwe kwa mujibu wa sheria siyo utashi wa viongozi.

“Kiongozi yeyote atakayekuja atalazimika kuilinda uhuru huu kwa mujibu wa sheria hata kama hataki,” amesitiza Nape na kuongeza kwamba hivi sasa mazingira ya wanahabari yako vizuri kwani hakuna waandishi ama watu wanaofungwa mdomo, hanna watu wanaofinywafinywanywa.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile amesema licha ya vyombo vya habari kuonekana kuwa huru, wadau wa sekta hiyo wanaamini kuwa uhuru zaidi utapatikana pale sheria ya huduma za vyombo vya habari itakapofanyiwa marekebishi.

Balile akizungumza katika kongamano hilo amesema serikali ya awamu ya sita imesadika kulegeza ugumu uliokuwa unaikabili sekta hiyo na kuvifanya vyombo vya habari kutokuwa huru.

Sekta ya habari wakati wa utawala wa Rais John Magufuli ilikumbwa na madhila kadhaa, makubwa yakiwa ni kuminywa kufanya kazi zao, kufungwa kwa magazeti, redio na televisheni, waandishi kufunguliwa kesi za uongo na kuwepo habari za waandishi kunyimwa haki ya msingi ya kuishi.

---

## **Walaani vifaranga hai kuchomwa**

**Na Scovya MANASE**

**V**ILIO vya vifaranga wa kuku 50,000 waliokuwa wakichomwa moto wakiwa hai, vimewaibuwa watetezi wa wanyama na viumbe, kulaani kitendo hicho walichokiita “cha kinyama.”

Vifaranga hao wa nyama na mayai walifikwa na vifo hivyo vya mateso walitotoleshwa katika shamba la kuku la Kibo Poultry liliko Manispaa ya Moshi, Kilimanjaro.

James Kamele, mwenyekiti wa Kituo cha Kutetea Wanyama Tanzania (TARC) ameliambia Pambazuko kwamba hatua ya kuu vifaranga hao kwa kuwateketeza kwa moto haikubaliki.

“Hao ni viumbe hai, hata kama ni wako, haikubaliki kuwaua kwa kuwatesa namna hiyo, halafu kibaya zaidi, unaita na waandishi wa habari wanapiga picha na kuziweka kwa umma,” alisema Kamele na kungeza – “hii haifai kabisa.”

Mwenyekiti huyo wa TARC amesema ungeweza kutumika utaratibu mwingine wa kuwaondolea uhai vifaranga hao, tena kama wanauma ama kunatishio la kusambaza ugonjwa, lakini siyo kukosa soko.

Amesema mmiliki wa shamba hilo angeweza kugawa vifaranga hao hata kwenye taasisi za elimu, ikiwamo shule, vyo na hata makanisani.

Mmiliki wa shamba hilo la kuku, Faye Crane amesema kwamba walifikia uamuzi wa kuwaua vifaranga hao kwa kuwachoma moto kwa kuwa “wamekosa soko la kuwauza.”

Faye amesema kampuni yake imekuwa ikizalisha kuku wengi na kwa zaidi ya miezi mitatu sasa, soko limekuwa “baya kiasi cha kukatisha tamaa na hata kushindwa kuendelea na biashara.”

Meneja uzalishaji wa shamba hilo, Vaileth Edward amesema kuwa kwa kipindi cha mwezi mmoja – kuanzia Oktoba hadi Novemba, mwaka huu,



wameua vifaranga mara mbili. Hata hivyo, idadi ya waliochoma mara ya kwanza hakuitaja.

Mtetezi mwingine wa wanyama na viumbe hai, Juma Awelimo, mkazi wa Mabwepande, Dar es Salaam, ameliambia Pambazuko kuwa pamoja na kuwepo kwa changamoto ya soko la vifaranga, bado kuwaua kwa kuwateketeza haukuwa uamuzi sahihi.

Amesema vifaranga hao wangeweza kugawiwa kwa watu wenye uwezo wa kuwatunza, na hasa majirani wa shamba hilo ili kujenga zaidi ujirani mwema.

Wenye wa shamba la kuku la Kibo wamelalamikia kuwepo kwa vifaranga kutoka nje ambao wanaingizwa nchini na kuuzwa bei ya chini zaidi kuliko bei yao.

Faye ambaye anajulikana zaidi kwa jina la Mama Kuku kutokana na kufanya biashara hiyo kwa muda mrefu, amesema kilio cha wazalishaji wengi wa kuku ni gharama kubwa za kuwatotolesha na kuwatunza vifaranga – hasa bei ya vyakula.

Rais wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliungana na idadi kubwa ya Watanania Novemba 28, 2021 kulaani vifaranga kutoka Kenya kuchomwa moto kwa kusema; “dhambi tupu viumbe wa Mungu mnamwaga petroli mnachoma, haukuwa na maana.”

## **Demokrasia ya kweli haina mapambio**

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

**T**UNAPOANGALIA nguzo za msingi za demokrasia. Ni vyema kukumbuka kwamba demokrasia ni uwepo wa nguzo hizo zote katika madaraja mbalimbali ya utawala.

Nguzo hizi zinaweka kipimo cha kinadharia juu ya jinsi mambo yanavyotakiwa kuwa. Mfano, tungeweka ubao wa kutolea alama za kupima jinsi kila nguzo ilivyotimizwa katika kila taifa au taasisi, basi tungepata picha ya utekelezaji kidemokrasia.

Katika utawala wa taifa tulizungumzia mihimili mitatu ya serikali ambayo ni utawala, bunge na mahakama. Mihimili hiyo yaweza kuwepo, lakini katika utendaji isiwe na tija katika kuboresha maisha ya raia. Mihimili hiyo yaweza kuwa klabu za wenye nguvu za kukandamiza haki za raia.

Sifa pekee zinazoweza kuleta tofauti ni hizo nguzo za demokrasia. Nguzo za demokrasia ndio huongeza thamani ya utawala wowote. Ndizo hushikilia kwa sehemu kubwa dhana nzima ya utawala bora. Nguzo za demokrasia ndio hufafanua demokrasia yenyewe.

Tunapoutazama uongozi wowote na kufanyia tathmini kwa misingi ya nguzo hizo, ndipo tunaweza kuweka kiasi cha demokrasia katika taasisi zeyote.

Tunaweza kutumia kipimo cha kuanzia sifuri mpaka kumi. Sifuri hapo ni kipimo cha uongozi usiokidhi kigezo cha nguzo yeyote katika kiwango chochote. Hapa tunaona utawala wa kidikteta uliokithiri.

Ambapo alama kumi ni uongozi wa kufikirika ambao hutimiza vigezo vya nguzo zote pasipo upungufu wowote. Huu ni utawala wa kidemokrasia wa kiwango cha juu.

Tunapoangalia nguzo hizi ndani ya kila mhimili wa serikali, tunaweza kujuliza maswali kadhaa, je, inawezekana mhimili mmojawapo wa serikali (kwa mfano



*Mikono*

bunge) ukaongozwa kidemokrasia ambapo miwili mingine haiendeshwi hivyo? Je, mhimili mmoja au miwili inapokuwa ya kidemokrasia, serikali yote imepata sifa ya kuwa ya kidemokrasia?

Serikali huwa ya kidemokrasia pale ambapo mihimili yote huendeshwa kidemokrasia. Demokrasia inatakiwa kuwa kama wimbi la bahari ambalo likipita hunyanyua juu mashua zote.

Tena ieleweke kwamba tunapozungumzia mihimili mitatu ya serikali hatuzungumzii serikali tatu, bali serikali moja katika mihimili mikuu mitatu ya utendaji. Huu ni mgawo wa wajibu kwa ajili ya utawala bora na utendaji wenye ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Kwa hiyo, ni muhimu nguzo hizo za demokrasia zionekane kama utandu wa buibui katika maisha na utendaji wa mihimili yote siku kwa siku.

Ni muhimu ziwepo katiba na sheria zenye nguvu ya kuonyesha hivyo na ambazo ni rahisi kusimamiwa. Tena ni muhimu iwepo nia ya dhati ya kujenga utawala wa kidemokrasia badala ya kujenga utawala wa kuibiana mapambio ya sifa bandia kila kukicha.

Ilipo demokrasia yenye taji la nguzo hizo muhimu, hakuna haja ya kutafuta maneno ya kusifu watawala, bali uongozi wao bora utawapa sifa na heshima.

---





**Na Evarist Chahali**  
evarist@chahali.com

## Takukuru imekwama, ijitathmini

**L**EO ni siku 10 kamili kwa “Tanzania” kutimiza miaka 61 tangu izaliwe Desemba 9, 1961 na kujiondoa kwenye kwapa za mkoloni Muingereza.

Nimeandika “Tanzania” kwa sababu kuna mjadala mkali unaoendelea kuhusu “uhuru wa Tanzania”. Kuna idadi kubwa tu ya watu wanaohoji kama kulikuwa na nchi inayoitwa Tanzania mwaka 1961, na wanaamini kuwa Desemba 9 ni maadhimisho ya “uhuru wa Tanganyika”.

Wanaopinga hoja hiyo wanasema “hakuna nchi inayoitwa Tanganyika kwa sasa.

Hata hivyo, lengo la makala haya siyo kuendeleza mjadala huo wala kuhukumu upande upi upo sahihi, ila nimeamua kuzungumzia moja ya changamoto kuu zinazoikabili Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; tatizo sugu la rushwa.

Japo ni kweli kwamba tatizo hilo lipo takriban kila nchi duniani, kwa sababu linahusu zaidi tabia ya mtu binafsi, kwa nchi nyingi za dunia ya tatu, ikiwa ni pamoja na yetu, rushwa imeota mizizi na kuwa sawa na mfumo wa maisha ya kila siku.

Niliwahi kusoma matokeo ya utafiti mmoja uliofanyika nchini mwetu miaka kadhaa iliyopita, ambapo zaidi ya nusu ya idadi ya wahojiwa walibainisha kuwa “rushwa imekuwepo tangu zamani hizo na itaendelea kuwepo”, “rushwa inasaidia na kuwezesha kupatikana kwa huduma haraka zaidi,” “rushwa inawasaidia wenye kipato duni kumudu maisha yao.”

Nakumbuka nilipokuwa mtumishi wa taasisi fulani nyeti serikalini, kijana mmoja aliyepata nafasi ya kuwa mhasibu “alichekwa” kwa “kupanda basi la ofisi badala ya kuwa na gari lake mwenyewe.” Kijana huyo alidhihakiwa kwa kuzongwa na maneno kuwa “anaishi kama siyo mhasibu.”



**Mkurugenzi Mkuu Takukuru, Salum Hamduni**

Na miaka kadhaa baadaye alipoanza kununua magari ya kifahari na kujenga hekalu nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, akaanza kumwagiwa sifa.

Majuzi nimemsikia Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiagiza Taasisi ya Kupambana na Kuzuwua Rushwa (Takukuru) ifanye uchunguzi katika maendeleo ya ujenzi wa miradi ya Hospitali ya Manispaa ya Sumbawanga na Kituo cha Afya cha Matanga, Rukwa ambapo tayari serikali imeshatoa zaidi ya shilingi bilioni mbili.

Nikajiuliza, kwanini suala hilo lisubiri maagizo ya Waziri Mkuu ilhali kuna ofisi za Takukuru huko Sumbawanga?

Ukweli mchungu ni kwamba taasisi hiyo imekuwa ikisuasua sana katika kuzuia na kupambana na rushwa, na hilo limechangia tatizo hilo kuzidi kuota mizizi.

Nihitimishe makala haya kwa kuwasihii Takukuru wajitathmini, lakini pia kuisihi serikali kuangalia uwezekano wa kuifumua taasisi hiyo iwe na ufanisi zaidi.

## **Mwakili waja kusaidia manusura**

### **Na Waandishi WETU**

**HAMPUNI** saba za mawakili kutoka mabara matatu; Afrika, Amerika na Ulaya zinaendelea kupishana - kwa kuhaha kupata ridhaa ya manusura wa ajali ya ndege ya Precision Air ili kutetea haki zao za fidia.

Mbali na manusura hao, kampuni hizo pia zinafanya jitihada za kupata ndugu na jamaa za abiria waliopoteza maisha katika ajali hiyo iliyotokea Novemba 6, 2022 baada ya kutua Ziwa Victoria, mita zinazokadiriwa kuwa 150 kutoka Uwanja wa Ndege wa Bukoba, Tanzania.

Pamoja na kwamba sababu halisi ya ajali hiyo bado haijatangazwa kwa umma, inaaminika kuwa hali mbaya ya hewa katika maeneo jirani na uwanja huo, ndiyo sababu kubwa ambapo watu 19 walifariki dunia, huku 24 wakinusurika.

Kampuni mbili zinatoka Marekani na moja Canada (Amerika); moja Tanzania (Afrika); na tatu kutoka Uingereza (Ulaya).

Kampuni hizo za mawakili ambazo bado zinaendelea na ushawishi wa manusura hao na ndugu wa waliopoteza maisha, zimekuwa zikipishana kuwasilina na wahusika ili kupata ridhaa ya kutetea maslahi yao ya fidia.

Pambazuko linazo taarifa za uhakika kuwa hadi sasa kampuni mbili za mawakili kutoka Marekani zimekutana na manusura ana kwa ana katika miji ya Dar es Salaam, Bukoba (mkoani Kagera) na Mwanza.

Moja ya kampuni hizo kutoka New York, Marekani ambayo baada ya kuwasiliana na Pambazuko imekataa kutajwa kwa sasa, ikieleza sababu ambazo imedai zinaweza kuharibu mchakato wao, imebainika kufika katika miji hiyo na kuzungumza na manusura.

Kampuni hiyo, ikiwakilishwa na mawakili wawili, ilifika Tanzania Novemba 25, 2022 na siku iliyofuata – Novemba 26, mawakili wake walikutana na waguswa wa ajali hiyo jijini Dar es Salaam. Mkutano wao ulihudhuriwa na waguswa tisa na mmoja aliwakilishwa

na ndugu baada ya kushindwa kufika kutokana na kuendelea kutibiwa. Mkutano huo ulifanyika Hoteli ya Hyatt ukumbi wa Bagamoyo.

Siku iliyofuata, mawakili hao walikwenda Mwanza na kufanya kikao na waguswa wa ajali hiyo wapatao wanne; mmoja aliwakilishwa na ndugu baada ya kuomba udhuru kwamba anaendelea kuumwa na hali zao siyo nzuri. Mkutano wao ulifanyika Hoteli ya Malaika Beach.

Baada ya kumaliza kikao na waguswa, mawakili hao walikwea ndege siku hiyohiyo na kufika Bukoba na kuweza kufanya kikao na waguswa sita katika Hoteli ya Victorious.

Mawakili hawa waliwaeleza waguswa kwamba sababu kubwa ya ujio wao ni kuwapa mwanga wa stahiki zao baada ya kutokea kwa ajali na kwamba – “dunia nzima, fidia halali na halisi ya ajali, hupiganiwa, kwani walipaji hupenda kulipa kidogo...” Hivyo wao wapo kusaidia.

Pambazuko limeweza kuzungumza na baadhi ya manusura ambao walihudhuria mikutano hiyo, wengi wakieleza kuwa “wamepata mwanga wa kutosha” kuhusu stahiki za waguswa wa ajali za ndege, siyo Ulaya tu, hata Afrika na chache zilizowahi kutokea Tanzania.

“Hawa mawakili waliotufikia uso kwa uso wameeleza mengi, na hakika tumepata ufahamu wa kutosha kuhusu fidia zetu, lakini inavyoonekana wanataka walipwe na sisi kutoka sehemu ya fidia, wakati wengi tuliaini wanalipwa na Precision,” ameliambia Pambazuko mmoja wa waguswa hao aliyeko Mwanza.

Waguswa wengine waliozungumza na Pambazuko – kwa masharti ya kutotajwa majina wamesema lugha ilikuwa kikwazo kuweza kupata lugha rahisi ya kuelewa kilichokuwa kikizungumzwa na hasa namna ya kutambua nani anatakiwa kupata nini na lini fidia itafika kwao.

Mawakili waliowafikia waguswa hao walikuwa wakitumia Kiingereza, huku

## Mawakili waja kusaidia manusura

wakiwa na mawakili kutoka Dar es Salaam wakifanya ukalimani.

“Lugha ilikuwa mgogoro na hatukuweza kuuliza maswali mengi zaidi, lakini waliosaidia kutafsiri, walisaidia, ingawa siyo kwa kiwango kinacholingana na kama tungekuwa wote Waswahili,” anasema mguswa huyo.

Mbali na kampuni hiyo kuwafikia uso kwa uso, mawakili wengine kutoka Marekani waliwafikia waguswa mmoja mmoja, nyumbani kwao na baadhi ofisini na kufanya mazungumzo yenye sababu ileile ya nia ya kusaidia kupatikana kwa stahiki kwa waliopata ajali ya Precision Air.

Imafahamika kuwa kampuni kutoka Marekani, Canada na Uingereza zinashirikiana na mawakili wa Tanzania kuwafikia waguswa, ingawa kampuni moja kutoka Dare s Salaam, imeamua kusimama peke yake kwa maelezo kuwa ina uzoefu katika kusimamia mashauri ya bima za ajali.

Mbali na kampuni mbili kuwafikia waguswa wa ajali hiyo, mawakili wengine wote wanawafikia kwa njia ya simu na barua-pepe. Pambazuko limepata kuona baadhi ya barua ambazo zinaandikwa kwa waguswa hao kutoka kwa mawakili.

Kila barua iliyoonwa na Pambazuko inaeleza namna mawakili wa kampuni husika walivyopambana kuwapatia fidia baadhi ya manusura wa ajali za ndege na kwamba “bila mawakili” kuna uwezekano mdogo wa kupata stahiki na halali za waliokumbwa na ajali za ndege kutoka mashirika ya bima.

Moja ya kampuni kutoka Uingereza ni Sterwards Law ambayo imesema inashirikiana na mawakili wa kampuni inayoongozwa na Jaji (mstaafu) Fakihi Jundu na Adadi Rajabu kuomba ridhaa ya waguswa kuwatetea.

### Malipo wanayoomba mawakili

Katika barua zote za mawakili hao ambao wanataka kusaidia waguswa wa ajali hiyo ya ndege kupata haki zao za malipo ya bima, wanaonyesha kutaka kulipwa asilimia 33 ya malipo ya fidia kwa kila mtu atakayepata.

Pambazuko limeona kampuni moja tu



*Ndege ya Precision ikiopolewa siwani*

ambayo inaeleza kulipwa asilimia 31 – ikiwa ni ile kutoka Tanzania, wakati zote zinazotoka Ulaya na Amerika zinataka kulipwa asilimia 33.

Kampuni hizo zinaeleza kuwa kiwango hicho ndiyo “standard” ya dunia na kwamba kinajumuisha shughuli zote ikiwamo kuhudhuria kwenye mashauri bila kukosa na bila kujali ni kwa muda gani, gharama za kuandaa shauri na utetezi, karatasi, nauli na mambo mengine muhimu katika kusimamia mashauri ya kisheria.

Hii maana yake ni kwamba endapo mguswa wa ajali atalipwa Sh. milioni 12 (milioni kumi na mbili) kampuni ya mawakili italipwa na mguswa Sh. 3,960,000 (milioni tatu na laki tisa na elfu sitini).

Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware amesema kuwa Precision Air iliyopata ajali imekatiwa bima hivyo inaweza kulipwa fidia inayofikia dola milioni 50 (50,000,000) sawa na shilingi bilioni 116 (116,000,000,000).

Pia, Saqware amesema kwamba - kwa pamoja, waathirika wa ajali hiyo watalipwa fidia ya dola zipatazo milioni 170, sawa na shilingi 396,000,000,000.

Asilimia 33 ya shilingi 396,000,000,000 ni sawa na shilingi 130,680,000,000.

## ...Waguswa waanza kulipwa milioni 11.7/-

**M**ANUSURA katika ajali na ndege ya Precision Air iliyotokea Novemba 6, mwaka huu – nje kidogo ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba, wameanza kulipwa malipo ya awali ya Sh. milioni 11.7.

Akizunguma na gazeti la Pambazuko jana jijini Dar es Salaam, mmoja wa wakurugenzi wa Precision Air alisema “ni kweli tumewapeleka mawasiliano ili wakubali kuanza kulipwa.”

Huku akikataa kutajwa jina gazetini kwa maelezo kuwa upo utaratibu wa kupata taarifa zote za ajali ile, aliongeza; “itambulike haya ni malipo ya awali.”

Pambazuko limeona baadhi ya nyaraka zilizotomwa kwa waguswa wa ajali ya ndege hiyo; ikiwemo barua ya Desemba 7, 2022 kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Precision Air, Patrick Mwanri na hati ya malipo.

Barua hiyo kutoka kwa Mwanri kwanza inawapa pole familia za abiria waliopoteza maisha na kuwatakia manusura kupona haraka.

Mwanri katika barua yake anaeleza kuwa malipo hayo ya dola za Marekani 5,000 ni “kusaidia matumizi ya haraka ya matibabu na huduma zingine za maisha.”

Hati hiyo ya malipo inawataka watakaokubali malipo hayo ya awali kujaza fomu maalum ambayo inaeleza kiasi na kwamba hayo ni malipo ya awali.

Hati hiyo inaeleza kuwa mpokeaji anapewa malipo hayo kutoka kwa Precision Air pamoja na/au kampuni za bima zinazohusika kama malipo ya awali (Malipo ya Awali) na kwamba hati hiyo ya kupokea malipo itakuwa halali baada ya ‘Malipo ya Awali’ kufanyika.

Kwa mujibu wa kanuni ya 31 wa Kanuni za Mamlaka ya Anga Tanzania

<b>HATI YA KUPOKEA</b> Ajali ya Ndege PW494 6 November 2022	
Mimi, .....	[andika jina lako]
wa .....	[andika anuani yako]
mwenye kitambulisho.....[taja aina ya kitambulisho na namba ya kitambulisho] abiria wa ndege ya Precision Air PW494 ya tarehe 06 November 2022, nakiri kupokea dola za kimarekani \$5,000/= au fedha za kitanzania zenye thamani ya dola za kimarekani \$5,000/=kwa kiwango cha kubadilisha fedha cha benki kuu ya Tanzania) kutoka kwa Precision Air pamoja na/au na kampuni za bima zinazohusika kama malipo ya awali (Malipo ya Awali) na hati hii ya kupokea itakuwa halali baada ya Malipo ya Awali kufanyika.	
Ninakiri nakukubali kupokea Malipo ya Awali kwa masharti yafuatayo:	
1. Malipo ya Awali yanafanywa kwa kuwezesha kukidhi mahitaji yangu ya kiuchumi ya haraka	
2. Kwa mujibu wa kanuni ya 31 wa Kanuni za Mamlaka ya Anga Tanzania (Usafiri wa Anga) 2008. Malipo ya Awali yanajumuisha malipo ya awali yatakayotolewa katika kiwango cha ziada kitakacholipwa na Precision Air pamoja na/ au kampuni zake za bima kama fidia kutokana na majeraha na madhara nliyoyapata katika ajali ya ndege PW494 iliyotokea Bukoba tarehe 6 Novemba 2022 kutokana na (a) tuzo yoyote itakayotolewa kupitia hukumu yoyote, au (b) suluhu yoyote itakayofanyika siku za usoni	

^ Haya Malipo ya Awali hayaathiri utetezi wa Precision Air  
^--hukika ikiwa ni pamoja na--

(Usafiri wa Anga) za mwaka 2008, Malipo ya Awali yanajumuisha malipo yatakayotolewa katika kiwango cha ziada kitakacholipwa na kampuni ya ndege pamoja na/au kampuni zake za bima kama fidia kutokana na majeraha na madhara aliyoyapata mhusika katika ajali ya ndege.

Mwanasheria Hamisi Kuleza ameliambia Pambazuko kuwa malipo hayo ya awali hayaathiri utetezi wa Precision Air au kampuni za bima zilizohusika ikiwa ni pamoja na matumizi ya pingamizi lolote linalowasilishwa na mguswa au taasisi yoyote.

## Likizo zijenge tabia njema



*Msazi akifundisha mtoto namna ya kufagia. Katuni ya The Citizen.*

### Na Tryruckia MFINANGA

**M**APUMZIKO ya mwisho wa mwaka hayawapi nafasi waajiriwa pekee kupumzika, bali watoto wa shule nao hupata muda wa kuwa nyumbani kwa muda wa zaidi ya mwezi mmoja.

Ileweke kuwa muda mrefu – kwa mwaka mzima, watoto wanakuwa shuleni, huku wazazi (wengi) wanakuwa kazini wakitafuta maisha ya familia zao na wale wanaowategemea.

Watoto wanapokuwa shuleni kazi kubwa ni kusoma, lakini pia hufunzwa mambo mengine mengi ya kuja kukabiliana na maisha; hufundishwa tabia njema, hufunzwa namna ya kuishi na jamii, hupata mwanya wa kukaa na wengine – kutoka familia na kada tofauti za maisha.

Mara nyingi, watoto wanapokuwa shuleni, hujenga tabia ya woga kwa kuwa wanatambua walimu wanaweza kuwaadhibu wanapokwenda kinyume na sheria za shule na taratibu zingine,

lakini hufungua tabia zao halisi wakiwa nyumbani.

Ndiyo maana katika kipindi hiki, wanapokuwa nyumbani kwa mapumziko, ni vyema wazazi nao wakawa na muda wa kuzungumza na vijana wao, hivyo makala haya yanakusudia kuhimiza wazazi kuzingatia haya kuwa wapange muda wa kuwa nao kila siku – wasipende kurudi na kuondoka mapema watoto wakiwa wamelala.

Ni vyema wazazi wakaketi na watoto wao na kuwauliza juu ya changamoto alizokutana nazo akiwa shule.

Ni vyema mzazi akapata mwanya wa kujadiliana na mtoto wake kuhusu matokeo yake ya mitihani ya darasani kwa mwaka mzima na kuhoji kwanini amepata alama za chini na apongezwe pale alipofanya vyema.

Kijana lazima ahimizwe kwenda kanisani au msikitini na huenda muda huo ni mzuri wa kujifunza namna ya kushika namna nzuri ya kumtukiza Mungu.

---

## Askofu Ruwaichi kukusanya trilioni 1.9/- za mafrateri

**Na Deusdedith KAHANGWA**

**A**SKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Thaddeus Ruwaichi, (pichani) anatarajia kukusanya shilingi trilioni 1.9 kusomesha mafrateri 86 kwa kipindi cha miaka saba.

Katika harambee iliyofanyika hivi karibuni, tayari zimekusanywa zaidi ya shilingi milioni 46 kwa ajili ya kuwasomesha mafrateri hao wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Fedha hizo zilipatikana kupitia harambee iliyofanyika Desemba 9, 2022, katika Kanisa la Parokia ya Msimbazi, Dar es Salaam ikiwajumuisha waseminari wa zamani wa kanisa hilo.

Harambee hiyo iliyotanguliwa na Misa iliyowashirikisha waseminari wa zamani wanaoishi Dar es Salaam, kwa ajili ya “kumshukuru Mungu kwa malezi ambayo waliyapata seminarini.”

Askofu Ruwaichi, aliwatambua waseminari hao wa zamani kuwa ni hazina ya pekee kwa kanisa, na kuwaalika kuendelea kuwa “mwanga na chumvi ya ulimwengu,” kwa njia ya “karama zao na vipawa mbalimbali.”

Baada ya Misa, Askofu Ruwaichi, wasaidizi wake, waseminari wa zamani na wageni wengine walifanya mazungumzo” kwenye ukumbi wa “Kardinali Adams,” ulioko ndani ya Kituo cha Msimbazi na ndipo harambee hiyo ilifutia.

Kupitia mazungumzo hayo, Askofu Ruwaichi aliwaomba waseminari wa zamani kukubali kubeba “utume maalum” wa kuwasomesha mafrateri wa jimbo lake wapatao 86 kwa sasa.

Masomo ya mafrateri huchukua miaka saba, inayojumuisha miaka mitatu ya falsafa na miaka minne ya teolojia.

Frateri ni mseminari mkubwa ambaye hupata ushewaji na hatimaye upadre, baada ya kupitia mchakato mrefu wa kumuandaa.

Padre Vincent Mpwaji, Chansela wa Jimbo, alieleza kwamba gharama za msingi za kumsomesha frateri mmoja kwa



mwaka ni shilingi milioni 2.6.

Mseminari mmoja wa zamani, alilieleza Pambazuko kwamba, nauli, vifaa vya masomo, na vitenda kazi vya mafrateri hufikia wastani wa asilimia 20 za gharama za msingi, yaani sawa na shilingi 530,000 za Tanzania.

“Hivyo, gharama zote za kumsomesha frateri mmoja kwa mwaka mmoja ni shilingi milioni 3.130; kumsomesha frateri mmoja kwa miaka saba ni shilingi 21,910,000 za Tanzania; na gharama za kuwasomesha mafrateri 86 kwa miaka saba ni shilingi 1,884,260,000 za Tanzania,” alifafanua.

“Hivyo, kwa kuwa tuna waseminari wa zamani 950 waliosajiliwa kwenye kundi letu, lengo hili linaweza kutimia kama kila mseminari wa zamani atachangia, angalau wastani wa shilingi 23,612 za Tanzania kila mwezi,” aliongeza.

Hatimaye, waseminari wa zamani, walikubaliana kuunga mkono ajenda ya kuwasomesha mafrateri; na kwamba michango itatumwa kwenye lipa namba maalum au akaunti ya benki hii: Archdiocese of Dar es Salaam - Major Seminarians Fund, Account Number 00111500025102.

Michango taslimu shilingi 2,854,000 za Tanzania ilitolewa siku hiyo. Pia kuna ahadi za shilingi 43,600,000 za Tanzania zilitamkwa. Hivyo, fedha taslimu na ahadi zilizopatikana siku hiyo ni shilingi 46,454,000.

---

# **Pambazuko**

## **Gazeti la Pambazuko sasa kupokea matangazo**

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi kwa

kuwasiliana kupitia namba hii:  
**0744 768 263** au Barua- Pepe;  
[info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

*Karibu sana Pambazuko isaidie  
kupaisha na kupambazua  
huduma na biashara yako.*

---

## **Kikwete asaidie tunu za taifa**

**Na Tryruckia MFINANGA**

**M**WAKA 2005, Jakaya Kikwete Maligombea urais wa Tanzania, na akajitambulisha kwa kutumia kaulimbiu isemayo; ‘Maisha bora kwa kila Mtanzania.’

Hotuba zake kadhaa, nilizozisikiliza, zinafafanua kaulimbiu hii kwa kutumia maneno yafuatayo, kati ya mengine mengi.

“Dalili za maisha bora ni uhai tele; afya bora; elimu bora; usawa katika huduma; kupendana na majirani; marafiki waaminifu; kazi ya kukuwezesha kuweka mkate mezani; fursa ya kufanya mazoezi ya viungo; kusema ukweli; kuwajibika kwa jamii pana; na kupata stahiki zako popote,” alisikika akisema Jakaya Kikwete, (usanisi wangu).

Kwa maneno haya, japo ni ya kawaida sana, Kikwete alikuwa amefanya kazi kama mwanazuoni aliyebobea kwenye ‘falsafa ya tunu,’ yaani axiology. Kwa njia nyepesi, Kikwete alikuwa ametusaidia kutofautisha kati ya “tunu chanya” na “tunu hasi” zifuatazo, kati ya zingine:

Uhai na kifo, afya na maradhi, elimu na ujinga, haki na dhulumu, uadilifu na uovu, utulivu na uhalifu, utajiri na umaskini, demokrasia na udikteta, upendo na chuki, heshima na dharau, uhuru na utumwa, usawa na ubaguzi, na orodha inaendelea.

Hivyo, kama ningeambiwa kuipatia kichwa cha maneno aya hii, ningesema kwamba Kikwete anaongelea “tunu zinazoboresha maisha ya watu.”

Hivyo, leo Jakaya Kikwete ndiye mwanafalsafa wa wiki katika safu hii. Napenda, kupitia mawazo yake, tukumbushane kuhusu nafasi ya “tunu za binadamu” katika katiba ya nchi yetu.

Kwanza, nakumbusha kuhusu “tunu za msingi,” kama vile: hadhi ya ubinadamu, uhai, afya, elimu, michezo na burudani, urazini timamu, urafiki na haki. Na pili, nakumbusha kuhusu “tunu za mpito,”



*Dr. Jakaya Kikwete*

yaani chakula, makazi, amani, uhuru, mali, mazingira, nishati, na maji.

Kwa kawaida, imani ya jamii yenye haki na amani ni kama pambetatu yenye kitako cha utu, kimo cha tunu na kiegama cha haki na majukumu. Lakini, Katiba ya Tanzania (1977), haitaji kwa uwazi “Tunu za Taifa,” ambazo ni msingi wa haki na majukumu yaliyomo.

Hata Rasimu ya Katiba ya Bunge Maalum la Katiba na Rasimu ya Katiba ya Tume ya Warioba hazikuzibia pengo hili.

Rasimu ya Katiba ya Bunge Maalum la Katiba, inasema kuwa Tanzania itaenzi ‘Tunu za Taifa’ zifuatazo: ‘Kiswahili, Muungano, utu, udugu, amani, na utulivu.’ Na ilizikataa tunu zilizopendekezwa kwenye Rasimu ya Katiba ya Tume ya Warioba.

Napendekeza kwamba, Kikwete na wataalam wa falsafa ya tunu kuisaidia Tanzania kupata Katiba Mpya yenye kuonyesha bayana sura inayojadili kinagaubaga ‘imani ya taifa kuhusu utu, tunu, haki na wajibu na asisitize kwamba dhana hizi tatu hazitenganishiki.

---



## Zanzibar: Uhuru halisi ni upi?

Na Awadh SAID  
Zanzibar

**M**IAKA nenda rudi – siyo ndani ya Zanzibar pekee, bali maeneo mengi duniani, kumekuwepo na malumbano kuhusu uhuru halisi wa visiwa hivyo.

Wapo wanaodai kwamba uhuru wa kweli ni ule uliopatikana Desemba 10, 1963 na wengine wakidai huo ulikuwa bandia; kwamba uhuru halisi uliletwa na Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964.

Pamoja na kwamba kila upande unavutia eneo lake unaloamini, lakini kuna maswali mengi yanayopaswa kujibiwa ili kupata uhalali kwa wale wanaopinga kwamba Desemba 10, 1963 haukupatikana Uhuru wa Zanzibar.

Ikumbukwe kwamba Mzee Abeid Amani Karume wakati akiwasilisha risala yake rasmi akiwa Mkuu wa Upinzani katika Baraza la Taifa la Zanzibar (National Assembly) katika kuukaribisha Uhuru wa Dola ya Zanzibar Desemba 10, 1963 maneno yake yafuatayo yalimaanisha nini?

“Leo mwezi 10 Desemba, 1963, Zanzibar imekuwa huru. Hii leo sisi watu wa visiwa hivi tumepata haki ya kuchukuwa mahala petu kuwa ni Dola sawa na nyengine katika Umoja wa Nchi za Dola za Commonwealth. Kwa uchache, kuwa mwanachama katika umoja huo, kuna maana kwamba nchi hii ni huru chini ya mpango wa serikali ambayo msingi wake umejengwa juu ya kuendelea kwa ridhaa ya wananchi.”

Aidha, siku sita tu baada ya Zanzibar kukabidhiwa uhuru wake, Desemba 16, 1963 ilijiunga na Umoja wa Mataifa (UN) na ikakaribishwa rasmi kuwa ni mwanachama wa 112 wa umoja huo, je, UN chombo holela kiasi kwamba waridhie kujiunga kwa nchi ambayo ina uhuru bandia?

Ikumbukwe kuwa Zanzibar katika kujiunga kwake UN, hakuna mwanachama wa umoja huo aliyepinga tangu kuanza kwa mchakato wake kwenye Baraza la Usalama (Security



Abeid Amani Karume

Council) na kuishia Baraza Kuu (General Assembly).

Ombi la Zanzibar kujiunga na UN lilidhaminiwa na Uingereza, Ghana na Morocco. Hivi mataifa haya yanaweza kudhamini nchi yenye “uhuru bandia” ikubaliwe kuwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa?

Tuseme wote hawa walipigwa changa la macho wakaidhamini nchi yenye “uhuru bandia” kuwa Mwanachama wa UN? Baada ya Zanzibar kukubaliwa kuwa Mwanachama wa UN, Sierra Leone na Japan zilitoa hotuba za kuikaribisha Zanzibar ikiwa ni mwanachama mpya, je, nazo pia zilipigwa changa la macho?

Zanzibar ilikabidhiwa uhuru wake na Uingereza chini ya serikali iliyokuwa ya muungano wa vyama vya ZNP na ZPPP ikiongozwa na Mohammed Shante Hamad chini ya mfumo wa vyama vingi na upande wa upinzani ukiongozwa na chama cha ASP chini ya Mzee Abeid Amani Karume.

Hata hivyo, Januari 12, 1964 -

---

**Zanzibar: Uhuru halisi ni upi?***Inatoka Uk. 17*

Serikali ya ZNP na ZPPP iliyokuwa chini Shamte ikapinduliwa na ASP chini ya Mzee Karume. Serikali Shamte ilidumu kwa siku 33 tu tangu ikabidhiwe uhuru/serikali na ilidumu kwa siku 27 tu tangu Zanzibar iwe mwanachama wa UN.

Lakini hata baada ya kutokea Mapinduzi, Zanzibar iliendelea kuwa mwanachama wa 112 wa UN bila mabadiliko yoyote. Kwa nini Zanzibar “iliyopata Uhuru” Januari 12, 1964 haikuomba anachama kama nchi yenye uhuru wake kamili badala ya ule uhuru mwingine? Kwa vipi ASP walikubali kubakia na uanachama uliotokana na uhuru unaonezwa kuwa bandia?

Mapinduzi yalitokea Januari 12, 1964, lakini Zanzibar ilibakia kuwa mwanachama wa 112 wa UN hadi Mei, 1964 ambapo Zanzibar iliondolewa uanachama wake baada ya kuungana na Tanganyika na kutengeza Tanzania.

Na kupitia uanachama huo wa UN uliopatikana kabla ya Mapinduzi, Mzee Karume alimteua Hasnu Makame Mwita kuwa Balozi wa Zanzibar huko UN (akiwakilisha pia Marekani) akichukua nafasi ya Hilal Mohammed Hilal aliyeteuliwa na Shamte.

Mbona haikuletwa hoja kuwa ule ulikuwa uhuru bandia, hivyo ulizaa uanachama bandia na kwa maana hiyo Zanzibar ingeomba uanachama upya chini ya nchi huru?

Teleweke kuwa Zanzibar chini ya huo uitwao uhuru Bandia, ilitambulika na dunia kuwa ni Dola iliyokuwa na nafasi, haki na hadhi sawa na madola (nchi) mengineyo na ikatambuliwa rasmi kuwa ni huru. Je, dunia nzima ilizibwa macho wasigutuke kuwa ule ni uhuru bandia tu?

Marekani na China ni miongoni mwa mataifa makubwa na kwamba zilikuwa nchi za kwanza kutuma wajumbe rasmi kuziwakilisha kwenye sherehe za Uhuru wa Zanzibar wa Desemba 10, 1963, je, nazo pia zilipigwa changa la macho?

Zanzibar chini ya huo uhuru bandia iliteua mabalizi wake kuiwakilisha Dola ya Zanzibar (Sovereign State of

**Mohammed Shamte**

Zanzibar) kama ifuatavyo: Balozi wa UN na Marekani - Hilal Mohd Hilal na msaidizi wake kuwa Hassan Khamis Ameir (almaaruf Tiger).

Balozi wa Zanzibar nchini Uingereza na Jumuiya ya Madola aliteuliwa Omar Zahran Alhaj; Misri akawa Nassor Lemky na msaidizi wake, Mzee Ali Khamis Abdulla (aliyekuwa Spika wa Pili wa Baraza la Wawakilishi); Indonesia kukawepo msaidizi wa balozi, Ali Hassan Mwinyi (Balozi alikuwa hajateuliwa), je, nchi zote hizi hazikushtuka kuwa zinaingia mkenge kupokea mabalizi kutoka nchi yenye uhuru bandia?

Majibu ya maswali haya endapo yatapatikana na kujibiwa bila jazba wala kuweka uongo kwa maana ya kuharibu historia, basi mjadala huu unaweza kuendelea kwa maana ya kujengana na siyo kubomoa ili kuwepo kwa historia ya kweli ya Zanzibar na dunia kupata ufahamu wenye mantiki chanya.

---

## **Polisi acheni kupiga ramli**

**Mhariri,**

**N**AANDIKA barua hii kwa niaba ya makuruta tuliofukuzwa kutoka Jeshi la Polisi tukiwa bado mafunzoni.

Kupitia kwako, ninaamini wakuu wa jeshi hilo na viongozi wengine, hasa Wizara ya Mambo ya Ndani watasikiliza kilio chetu na ikiwezekana kuchukua hatua ili kukomesha unyanyasaji na kudhalilishwa kwa utu.

Makututa kadhaa tulifukuzwa kwa sababu ya tuhuma kwamba tuna vidole virefu na makalio makubwa hivyo kudhaniwa kuwa ni “mashoga.”

Napenda ifahamike kwamba vidole na viuno vyetu siyo vikubwa kama ilivyotangazwa. Na kama ingekuwa hivyo, jeshi lilipaswa kuchukua vipimo vya kisayansi na kitabibu ili kuthibitisha tuhuma zao kwetu, lakini hilo halikufanyika kamwe.

Uongozi wa jeshi hilo haukuchukua vipimo vya aina yoyote, isipokuwa kubebwa na hisia.

Hivyo, kufanya uamuzi kwa pupa kwa kutumia makisio ya kienyeji kama wapiga ramli wazushi; kwamba wenye vidole virefu na makalio makubwa, ni mashoga.

Wakubwa hawa wa jeshi wametumia sayansi batili ya zama za mawe wakati sayansi mamboleo zipo.

Kutokana na kuonewa, kudhalilishwa na kutwezwa utu wetu, tunaomba serikali, kupitia wizara husika kurudisha makuruta wote waliofukuzwa kwa tuhuma tu.

Ikiwezekana kabla ya kurudishwa, vipimo vya makuruta wote vichukuliwe na ukweli kwamba nani shoga na yupi siyo, ufahamike kisayansi.

**Aliyeonewa,  
Dodoma.**

## **Dawa zakosekana Amana**

**Mhariri,**

**K**UMEKUWEPO upungufu mkubwa wa dawa za magonjwa yasiyoambukiza, hasa Kisukari katika Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, Dar es Salaam.

Mimi ni miongoni mwa wagonjwa wa Kisukari ambao tumekuwa tukihudumiwa na hospitali hiyo kwa muda mrefu sasa, tangu mwaka 2019.

Katika kipindi cha miaka mitatu hivi, dawa za ugonjwa huo zilikuwa zikipatikana kwa wingi na mimi na wenzangu, hatukuwahi kuwa na shida ya kupewa dawa hizo, lakini kipindi cha mwaka mmoja uliopita, kumekuwepo na madadiliko.

Mara nyingi ukifika wakati wa kwenda

kupata dawa, unaeleza na wahusika kwamba hakuna dawa, sababu kubwa wakieleza kwamba hawajapokea kutoka serikalini.

Sasa najiuliza, hivi hii serikali imegoma kuagiza dawa za wagonjwa Kisukari? Je, kwanini iwe hivyo sasa au kuna mambo ya hovyo yanaendelea?

Naomba serikali ifatilie hili na ihakikishe dawa za magonjwa yasiyoambukizwa, hasa kwa sisi wazee, zinapatikana kwa wingi, siyo Mwananyamala tu, bali Tanzania nzima.

**Athumani Lugelo,  
Kinondoni,  
Dar es Salaam.**

### **Tunapokea Barua**

*Mhariri anapokea barua kutoka wasomaji wake kwa ajili ya kuzichapisha ama kuzitafutia majibu kutoka ofisi za serikali na binafsi. Tuma barua yako kwa njia ya barua-pepe: [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz) au kupitia namba ya simu: 0744 768 263*

---

**Misingi ya mapinduzi ya kifikra****Na Mwandishi WETU**

**K**UJENGA imani ya jamii ni kazi ya kubadilisha imani ya jamii kuhusu maumbile ya watu pamoja na mazingira yao, mifumo ya tunu, na mifumo ya majukumu.

Mwanafalsafa John Danaher, wa Chuo Kikuu cha Ireland, ametoa mantiki ya mabadiliko haya kupitia andiko lake, “A Taxonomy of Possible Moral Changes.”

Kimsingi, imani ya jamii ni kama umbo la pembetatu lenye kitako, kimo na kiegama. Kuna kitako cha imani kuhusu maumbile ya watu na mazingira yao, kimo cha imani kuhusu tunu, na kiegama cha imani kuhusu majukumu.

Hivyo, mfumo wa majukumu hutokana na imani ya jamii kuhusu maumbile ya watu na mazingira yao, pamoja na imani ya jamii kuhusu mfumo wa tunu. Kwa hivyo, tukitaka kupindua fikra za watu zilizopitwa na wakati, tunapaswa kufanya mabadiliko kwenye maeneo haya matatu. Nafafanua.

Mosi, mabadiliko kwenye imani kuhusu maumbile ya watu na mazingira yao ni mabadiliko kuhusu mifumo ya kada za vitu halisi na vitu visivyoyali.

Yanaweza kufanyika kwa kuibua kada mpya za vitu halisi duniani; kupangua na kupanga upya piramidi la kada za vitu halisi, na hivyo baadhi ya vitu kubadilishana nafasi; na kuhamisha vitu vilivyoyali kwenye kada za vitu halisi na kuvipeleka kwenye kada za vitu visivyoyali, au kinyume chake.

Pili, mabadiliko kwenye imani kuhusu mifumo ya tunu, ni mabadiliko kuhusu “tunu chanya na tunu hasi.”

Yanaweza kufanyika kwa kuibua tunu mpya; kupangua na kupanga upya piramidi ya tunu za kijamii, na hivyo baadhi ya tunu kubadilishana nafasi; na kuhamisha tunu zilizo kwenye seti ya tunu chanya na kuzipeleka kwenye seti ya tunu hasi, au kinyume chake.

Na tatu, mabadiliko kwenye imani kuhusu seti za majukumu, ni mabadiliko

*Prof. John Danaher*

na majukumu yenye sura ya ulazima, majukumu yenye sura ya ruhusa, majukumu ambayo ni makatazo na majukumu yenye uhiari.

Yanaweza kufanyika kwa kubuni na kuibua majukumu mpya; kupangua na kupanga upya piramidi ya vipaumbele vya majukumu yetu, na hivyo baadhi ya majukumu kubadilishana nafasi; na kuhamisha majukumu kutoka kwenye seti moja ya majukumu hadi kwenye seti nyingine ya majukumu, kama zilivyotajwa hapo juu.

Hata hivyo, John Danaher anasema kuwa, mabadiliko ya kijamii yatafanikiwa endapo kuna mfumo wa kufanikisha mabadiliko ya kifikra, na jamii iko tayari kubeba gharama ya uamuzi wa kuachana na tabia ya kubembeleza “urafiki wa Kaizari,” maana “wakubwa” wengi hawapendi mabadiliko.

---

## Washukumungu vs Wachamungu

Na Bruno MARCELO

**K**ATIKA dola ya kidemokrasia, kuna “miungu” wengi, kila “mungu” akiwa na jina lake. Mfano, kuna wafuasi wa “mungu” anayedaiwa kustaafu kazi baada ya kuumba ulimwengu, yaani, “deistic god” au “mungu deistika.” Kuna wafuasi wa “mungu” asiyestaafu kazi, yaani, “theistic god” au “mungu tehistika.”

Kuna wafuasi wa “mungu” ambaye ni “roho” iliyo ndani ya ulimwengu wa mwili, kama ambavyo, binadamu anao mwili na roho. Yaani, “pantheistic god” au “mungu pantehistika.” Na kuna “mungu” mwenye jina la “mtu” aitwaye “Mungu.”

Kwa hiyo tunapojadili hoja zinazohusu kuwepo au kutokuwepo kwa “mungu” lazima kubainisha aina ya “mungu” tunayemwongelea.

Katika makala zilizotangulia katika gazeti hili, pamoja na makala haya tunajadili hoja zinazomhusu “mungu tehistika,” kwa maana ya watu wanaokosoa hoja za kutetea uwepo wa “mungu tehistika.” Hawa ni watu wanaokosoa hoja ya kimaadili, hoja ya kiontolojia, hoja ya kikosmolojia, na hoja ya kiteliolojia.

Washukumungu wanatilia shaka hoja ya kimaadili, kwa sababu ya madai kwamba, kitendo kiovu, kama vile kuiba, kinakatazwa na “mungu” kwa sababu ni kitendo kiovu, lakini hakiwi kiovu kwa sababu “mungu” amekikataza.

Wanatilia shaka hoja ya kiontolojia, kwa sababu ya madai kwamba, kama vitu visivyoozeeka (abstract objects), kama vile “namba” na sifa ya “rangi” vipo, basi, vilikuwepo tangu milele yote, na hivyo, viko nje ya himaya ya “mungu,” kiasi kwamba “mungu” aliye mtawala wa kila kitu, hayupo.

Wanatilia shaka hoja ya kikosmolojia, kwa sababu ya madai kwamba, kama kila kitu kina mwanzo, chanzo cha “mungu” ni nini; na kwamba, kama kuna uwezekano wa “mungu asiyebadilika” kuwepo tangu milele yote, pia inawezekana



**Mawinguni**

jumla ya “uzito na nishati ya mfumo wa ulimwengu visivyobadiliki” vilikuwepo tangu milele yote.

Wanatilia shaka hoja ya kiteliolojia, kwa sababu ya madai kwamba, kwa mujibu wa Charles Darwin, nadharia ya mvuvumko inaweza kueleza mpangilio uliopo katika ulimwengu wa kibayolojia bila kutegemea maelezo ya “kimungu.”

Aidha, wafuasi wa “mungu deistika” wanatilia shaka hoja kuhusu “mungu tehistika” kwa sababu ya madai kwamba, uwepo wa kanuni za maumbile ni ushahidi kwamba, tayari “mungu” amepumuzika kazi.

Na wafuasi wa “mungu pantehistika” wanatilia shaka hoja kuhusu “mungu tehistika” kwa sababu ya madai kwamba, mungu aliye nje ya ulimwengu wetu, haweza kusababisha matukio yanayoleta mabadiliko hapa ulimwenguni.

Huo ndio mnyukano kati ya wachamungu na washukumungu na ambao umekuwa unaendelea kwa zaidi ya miaka 3000 sasa, na utaendelea milele.

---

## Utumwa ni uhalifu dhidi ya utu

Na Marious KAMELA

**D**ESEMBA 2, 1949, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Mkataba wa Kukomesha Biashara ya Watu.

Mwaka huu wa 2022, katika muktadha wa siku hiyo ya kimataifa ya kila mwaka, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, alitoa mwito kwa serikali na jamii kujipanga upya kwa ajili ya kutokomeza mabaki ya utumwa katika jamii.

Guterres alisema; “tunapoadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Utumwa, ni lazima tutambue kwamba athari za utumwa na biashara ya utumwa bado zinaendelea kuonekana duniani kote hivi leo na dunia ni lazima ichukue hatua zaidi kushughulikia athari hizo.”

Mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa (UN) pia alihimiza hatua zichukuliwe kutambua na kujitolea zaidi kutokomeza aina zote za utumwa wa kisasa, kuanzia kwa watu wanaofanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu hadi kwa ukatili wa kingono, ajira kwa watoto, ndoa za shuruti na matumizi ya watoto katika vita vya silaha.

Guterres alisema kuwa watu milioni 50 walifanywa watumwa katika kipindi cha mwaka jana.

Alisema kuwa, utumwa unajumuisha hali zote za unyonyaji ambapo mtu hawezi kukataa, au kuondoka, kwa sababu ya vitisho, vurugu, kulazimishwa, udanganyifu, au matumizi mabaya ya mamlaka.

Ujumbe wa katibu mkuu huyo ni kwamba, utumwa wa kisasa unatokea karibu kila nchi duniani, na unapita katika migongo ya kikabila, kitamaduni na kidini.

Kwa maana hiyo, Guterres alibainisha kwamba; “ni lazima pia tutambue na kutokomeza aina za utumwa mamboleo kama vile biashara haramu ya binadamu, unyonyaji wa kingono, ajira ya watoto, ndoa za kulazimishwa na matumizi ya watoto katika migogoro ya silaha.”

Makadirio ya hivi karibuni kuhusu utumwa mamboleo ulimwenguni juu



Antonio Guterres

ya kazi ya kulazimishwa na ndoa za kulazimishwa, yanaonyesha kwamba, mnamo 2021, watu zaidi ya milioni 50 walifanywa kuwa watumwa, na idadi hii inaongezeka.

Hapo zamani, kwa kawaida, soko la watumwa lilikuwa mahali ambapo watumwa wananunuliwa na kuuzwa.

Kuanzia miaka ya 1800 hadi 1890, soko la watumwa la Zanzibar lilikuwa kubwa kulizo masoko yote duniani. Kati ya watumwa 25,000 hadi 50,000 wa kutoka Afrika waliletwa ili kuuzwa kwenda pwani ya Somalia na sehemu nyingine na baadaye kusafirishwa Ulaya.

Wengi wao walitoka katika makabila ya Wamakua, Wanyasa, Wayao, Wazaramo na Wazigua ambao ni makabila ya Tanzania, Msumbiji na Malawi.

Mantiki ya biashara ya utumwa ni kwamba, Wazungu walikuwa watu kamili, Waasia nusu watu na Waafrika robo-mtu wanaohitaji muda mwingi ili waweze kufikia ustaarabu kamili wa kiutu.

---

## **Qatar imetia fora – FIFA**



*Moja ya uwanja uliotumika kwenye michuano ya Kombe la Dunia, Qatar, mwaka huu (The Mirror)*

### **Na Shabaan LULELA**

**S**HIRIKISHO la Soka Duniani (FIFA) limeeleza kufurahishwa kwake na maandalizi na hatimaye kufanikisha kufanyika kwa michuano ya Kombe la Dunia huko Qatar.

Hii ni mara ya kwanza kwa nchi kutoka eneo la Uarabu kuandaa mashindano hayo makubwa zaidi kwa upande wa soka kwa wanaume.

Rais wa shirikisho hilo, Gianni Infantino, Ijumaa iliyopita, akiwa Doha, Qatar alisema amefurahishwa kwa namna nchi hiyo yenye watu milioni tatu tu, iliyoweza kuandaa michuano ya kombe hilo kwa kiwango cha juu.

“Hakuna nchi iliyowahi kuandaa mashindano haya kwa ubora kama tulioshuhudia Qatar, kila kitu kimeenda sawa na kila hatua ilikuwa ni muda wa furaha kuanzia nje na hata ndani ya uwanja kushuhudia timu zikiumana kuwania ushindi,” amesema.

Kiongozi huyo alisema Qatar ilijipanga vyema kuanzia miundombinu ya kila mahali, viwanja vyenye hadhi kubwa na amani kila kona ya nchi hiyo yenye kimomita za mraba 11,000 tu.

Michuano ya kombe hilo iliyoanza kwa mara ya kwanza mwaka 1930, huko nchini Uruguay, inaelezwa kuwa aghali zaidi huku ikiwa imetumia zaidi ya dola za Marekani bilioni 220.

Infantino alisema ufanisi huo umeondoa dhana kwamba mataifa madogo kama Qatar hayana uwezo wa kuandaa mashindano makubwa ya kimataifa.

Mashindano hayo yaliyoingia mwaka wa 22 tangu kuasisiwa kwake yalizikusanya nchi 32 zilizoshindana tangu Novemba 20, mwaka huu.

Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa michuano hiyo kufanyika katika eneo la Mashariki ya Kati na ardhi ya Uarabuni kwa mara ya kwanza.

Katika michuano ya mwaka huu, mechi moja imekuwa ikivutia mashabiki 52,760, wakati idadi ya juu zaidi ikifikia 88,666 wakati wa mechi ya Kundi C kati ya Argentina na Mexico iliyochezewa Uwanja wa Lusail. Karibu mashabiki milioni 4 wanajadiriwa kuingia viwanjani wakati wa michezo hiyo.

Michuano hiyo pia ilifanyika kwa mara ya kwanza katika ardhi ya Afrika mwaka 2010 nchini Afrika Kusini.

**WANAUME 46. MWANAMKE 1. NI SAMIA!**



*Takriban viongozi 50 kutoka nchi za Afrika walikaribishwa Washington DC katika mkutano na Rais wa Marekani na Rais Joe Biden kujadili mambo kadhaa ikiwamo namna bora ya kushirikiana katika maeneo ya usalama, uchumi na biashara. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alihudhuria huko na kupata fursa ya kuzugumza na Rais Biden na wakuu wengine wa taasisi na mashirika walioko Marekani. Mkutano huo ulifanyika Desemba 13, 2022. Katika picha hii, Rais Dkt. Samia ndiye mwanamke pekee akiwa kiongozi wa nchi. Anaonekana akiwa ni wa kwanza kutoka kushoto waliosimama nyuma kabisa. (Picha: Ikulu ya Marekani).*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

